**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

Telephone: (028) - 2642830
Fax: (028)-2640235
Email: maravtc@veta.go.tz

VETA MARA
P. O. Box 188
MUSOMA
MARA - TANZANIA

## MKATABA WA FUNDI – LOCAL FUNDIS' CONTRACT

1. Mkataba huu umefungwa leo Siku ya ..10.... Mwezi wa ..01.... Mwaka 2022 Kati ya Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha ....VETA......., S.L.P. 188 MUSOMA ambacho kinawakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA Mara S.L.P. 188, Musoma. (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja

**NA**

EDWARD JONAS MAREGESI S.L.P. ..601..., MUSOMA.........
(ambaye katika mkataba huuatajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine

KWA KUWA, Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya UFUNGAJI WA BRANDERING NA UFUNGAJI WA MIKANDA - KARAKANA YA UASHI NA UMEME.

**KWAMBA**

2. Mwajiri amekubali zabuni/maombi ya fundi ya kufanya kazi, kuimaliza na kurekebisha makosa yote yatakayojitokeza
3. Katika mkataba huu maneno na maana yake ni sawaa na kama ilivyo kwenye sheria za mikataba ya majenzi; Ankra ya gharama na michoro vitatumika kama sehemu ya mkataba huu.
4. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kwa kadri ya mahitaji ya fundi hadi kazi itakapokamilika.
5. Fundi atatoa nguvu kazi inayotakiwa (Vibarua), Chakula na vifaa vya ufundi wake kutenda kazi hiyo na kuimaliza kwa wakati
6. Vitendo vya wizi wowote haviruhusiwi kabisa eneo la kazi katika kipindi chote cha mradi.
7. Mwajiri atamlipa Fundi gharama za ufundi, ndani ya siku kumi na nne baada ya kuomba malipo kwa 10% ya malipo ya awali, kazi ikikamilika kwa 20% atamlipa 15% ya gharama za ufundi, kazi ikikamilika kwa 50% atamlipa 20% ya gharama ya ufundi, kazi ikifika kwa 80%

atamlipa 30% ya gharama ya ufundi na kazi ikakamilika kwa 100% atamlipa 20% ya malipo ya ufundi. hivyo kwa kila hatua ya Ujenzi itakayokamilika kama inavyosomeka atalipwa jumla ya Tshs 1,000,000/= (MILIONI MOJA TU.)

8. Fundi anatakiwa kuwalipa vibarua aliowaajiri mara baada ya kupokea malipo ya kazi waliofanya kutokana na makubaliano yao.
9. Kuzingatia na kutekeleza masharti yote ya sheria za nchi zinazohusiana na kazi anayoifanya.
10. Kukubali kukatwa na mwaajiri kodi ya zuio (witholding tax)

**KWAMBA**

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHA ***VETA MARA***

Jina: DAVID LOUIS Saini ..........

Wadhifa: MSIMAMIZI WA MRADI Tarehe 10/01/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ALFRED G KUDIFU Saini ..........

Wadhifa: AFISA MANUNUZI MSAIDIZI Tarehe 10/01/2022

FOR. CENTRE PRINCIPAL MARA VTC P.O. BOX 188 MUSOMA

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: EDWARD JOHN MAREGESI Saini ..........

Wadhifa: FUNDI MKUU Tarehe 10/01/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: THOMAS KISHARA Saini Kishara

Wadhifa: SHAIDI Tarehe 10/01/2022